JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

MISITU NI MALI

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MNADA WA KIELEKTRONIKI

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza miti aina ya misaji yenye jumla ya meta za ujazo **10,721.909** iliyopo katika Shamba la miti Mtibwa lililopo Turiani Mkoani Morogoro na shamba la miti Longuza, Muheza Mkoani Tanga. Jumla ya meta za ujazo **5,188.04** na **5,533.87** zitauzwa katika Shamba la miti Mtibwa na Longuza mtawalia.

1. Miti ya Misaji itauzwa kwa njia ya mnada wa kielektroniki kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Misitu za Mwaka 2004. Mnada huu utafanyika siku ya **Jumatatu** tarehe **11 Disemba, 2023** kuanzia saa mbili kamili (02:00) asubuhi hadi saa sita na dakika thelethini na mbili (06:32) mchana kwa Shamba la miti Mtibwa na **Jumanne** tarehe **12 Disemba, 2023** kuanzia saa mbili kamili (02:00) asubuhi hadi saa nane na dakika hamsini na moja (08:51)mchana kwa Shamba la miti Longuza.

2. Ili kushiriki kwenye mnada, mshiriki atatakiwa kujisajili kupitia anuani ifuatayo http://mis.tfs.go.tz/e-auction kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi saa tano kamili (5:00) usiku wa tarehe **9 Disemba 2023** siku ya **Jumamosi.** Kwa ajili ya msaada wa usajili, wasiliana na: +255 713 335 926 or +255 766 857 062.

3. Washiriki wanakaribishwa kukagua miti iliyopo shambani wakati wa saa za kazi; kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Ukaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe ya Tangazo hili hadi tarehe **8 Disemba, 2023** siku ya **Ijumaa**. Wahifadhi wakuu wa Mashamba husika au wasaidizi wao watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada.

Masharti ya kushiriki Mnada huu

Mshiriki anapaswa kujisajili na kuthibitisha ushiriki wake na hivyo atakuwa amekubaliana na masharti yafuatayo: -

1. Kila Ploti itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo.

2. Baada ya kukamilisha usajili, mshiriki atatakiwa kuthibitisha ushiriki wake

angalau dakika tano (5) ambayo ni saa 01:55 asubuhi kabla ya muda wa mnada kuanza.

Muhimu: Uthibitisho baada ya mnada kuanza hautakubaliwa.

3. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha baada ya kupokea hati ya madai (bill) ya Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itakayopatikana kwenye akaunti ya mshiriki kwenye mfumo wa mnada wa kielektroniki.

4. Mshiriki atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi baada ya siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo aliouziwa. Mnunuzi ataruhusiwa kulipia zaidi ya asilimia 25 ya malipo ya kitalu chochote mara tu baada ya kukamilisha malipo ya awali ya 25% kwa vitalu vyote alivyonunua. Asilimia sabini na tano (75 %) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia sikuya mnadi.

5. Mshiriki atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50 (1) ya kanuni za misitu za mwaka 2004.

6. Mshiriki aliyeshinda atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba au wasaidizi wake kama uthibitisho wa malipo siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

7. Mshiriki aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya miezi miwili (**siku sitini**) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100. Aidha, endapo kutajitokeza changamoto ambazo zitasababisha kushindwa kuondoa mazao hayo ya misitu kwa muda uliopangwa, barua rasmi itawasilishwa kumjulisha Mhifadhi Mkuu wa Shamba kwa maamuzi.

8. Miti hiyo ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo kufanyika.

Wajibu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

Wakala;

1. Utapanga ploti za kuuza kama zinavyooneshwa katika Jedwali la orodha ya bei za kianzio (mrabaha tu) kwa mita moja ya ujazo, na
2. Utatoa barua ya ushindi na hati ya madai kwa mnunuzi aliyeshinda mnada kwa kila ploti mara baada ya kumalizika kwa mnada.

Ploti za Miti ya Misaji inayouzwa

Ploti zimepangwa kwa mafungu, ambapo kila baada ya masaa mawili na robo(2:15) fungu moja litauzwa. Vilevile ndani ya muda wa mnada uliotengwa kutakuwa na mapumziko (waterbreak) ya dakika mbili kila baada ya fungu moja kuuzwa.

Ploti zinazouzwa zimeorodheshwa katika jedwali namba 1 na j edwali namba 2 kama ifuatavyo: -

JEDWALI Na. 1; ORODHA YA PLOTI ZITAKAZOUZWA KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA SIKU YA JUMATATU TAREHE 11 DISEMBA, 2023

Na.	JINA LA KIUNGA	UJAZO (M^3)	BEI PENDEKEZWA (Tshs/Cbm)	FUNGU LITAKALO UZWA
1	LR16A-30	472.621	365,000	Fungu Na. 1 kwa Masaa 2 na dakika 15
2	LR 16 A-33	462.151	300,000	
3	LR 16 A-34	306.935	300,000	
4	LR 16 A-35	442.266	300,000	
5	LR 16 A-36	366.010	300,000	
6	LR 16 A-37	255.487	180,000	
7	LR 16 A-38	260.584	250,000	
8	LR 16 A-39	467.758	250,000	
9	LR18-6	185.855	600,000	Fungu Na. 2 kwa Masaa 2 na dakika 15
10	LR18-7	365.291	600,000	
11	LR18-8	214.390	600,000	
12	LR18-9	232.641	600,000	
13	LR18-10	462.202	600,000	
14	LR18-11	169.416	600,000	
15	FN77_1	278.281	300,000	
16	FN77_2	246.158	320,000	
JUMLA		**5,188.04**		

JEDWALI Na. 2: ORODHA YA PLOTI ZITAKAZOUZWA KATIKA SHAMBA LAMITI LONGUZA SIKU YA JUMANNE TAREHE 12 DISEMBA, 2023

NA.	JINA LA KIUNGA	UJAZO (M3)	BEI PENDEKEZWA (TZS)	FUNGU LITAKALO UZWA
1	KH4-A1	164.473	780000	Fungu Na. 1 kwa Masaa 2 na dakika 15
2	KH4-A2	178.533	780000	
3	KH4-A3	200.545	780000	
4	KH4-A4	160.885	780000	
5	KH4-A5	103.053	780000	
6	KH4-A6	192.92	780000	
7	KH4-A7	149.721	780000	
8	KH4-A8	151.265	780000	
9	KH4-A9	120.307	780000	
10	KH4-A10	54.53	780000	
11	KH4-A11	86.756	780000	
12	KH4-A12	242.409	780000	
13	KH4-A13	160.792	780000	
14	KH4-A14	100.271	780000	
15	KH4-A15	127.224	780000	
16	KH4-A16	120.269	780000	
17	KH4-A17	185.444	780000	
18	KH4-A18	50.266	780000	Fungu Na. 2 kwa Masaa 2 na dakika 15
19	KH4-A19	140.6	780000	
20	KH4-A20	115.049	780000	
21	KH4-A21	95.062	780000	
22	KH4-A22	122.912	780000	
23	KH4-A23	146.426	780000	
24	KH4-A24	202.405	780000	
25	KH4-A25	135.213	780000	
26	KH4-A26	134.317	780000	
27	KH4-A27	103.961	780000	
28	KH1-C13	67.262	693000	
29	KH1-t25	79.719	500000	
30	KH1-C3	56.484	693000	
31	KH1-C4	65.239	693000	
32	KH1-C2	72.711	693000	
33	LG12-A2	94.936	370000	
34	LG12-A3	183.358	370000	
35	LG12-A4	121.568	370000	Fungu Na. 3 kwa
36	LG12-A7	132.966	370000	
37	LG12-A8	95.433	370000	
38	LG12-A9	74.187	370000	

39	LG12-A10	93.088	370000	Masaa 2 na dakika 15
40	LG12-A12	90.413	370000	
41	LG12-A15	55.378	370000	
42	LG12-A16	83.409	370000	
43	LG12-A18	40.814	320000	
44	LG12-A19	51.655	320000	
45	LG12-A20	50.571	320000	
46	LG12-A21	49.887	320000	
47	LG12-A22	70.856	320000	
48	LG12-A23	51.155	320000	
49	LG12-A24	39.125	270000	
50	LG12-A28	68.047	320000	
	JUMLA KUU	**5,533.87**		

Tangazo hili linapatikana katika tovuti zifuatazo za: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz

Limetolewa na;
KAMISHNA WA UHIFADHI
S. L. P. 2228
DODOMA